



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



Anuani ya Simu: "UCHAGUZI

Nambari ya Simu: +255 26-2962345-8

Nambari ya Nukushi: +255 26-2962348

Baruapepe: uchaguzi@inec.go.tz

Tovuti: www.inec.go.tz

Unapojibu tafadhali taja

Kumb.Na. SAB.74/75/01/20

Wakurugenzi wa Majiji wote,

Wakurugenzi wa Manispaa wote,

Wakurugenzi wa Miji wote,

Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya wote,

TANZANIA BARA.

Yah: **AJIRA ZA WAANDISHI WASAIDIZI NA WAENDESHAJI WA VIFAA VYA BAYOMETRIKI**

Kama mnavyofahamu, mwaka huu wa 2024, Tume itaendesha zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Katika zoezi hilo, moja ya watendaji wanaohitajika ni Mwandishi Msaidizi na Mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki (BVR Kit Operator). Watendaji hawa huwa wanaajiriwa kwa ajira ya muda na huwa wanapaswa kutoka katika Kata (Vijiji na Mitaa) ambako ndipo Tume huweka vituo vya kuandikisha wapiga kura.

2. Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 7(4) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024, watendaji wa uboreshaji ngazi ya kituo cha kuandikisha wapiga kura hupatikana baada ya Tume kuteua maafisa waandikishaji chini ya kifungu cha 7 cha sheria tajwa.

3. Kwa kuwa bado Tume haijateua maafisa waandikishaji wa jimbo na kwa kuzingatia kifungu cha 7(4), utaratibu utakaotumika kuwapata watendaji ngazi ya kituo ni kama ifuatavyo: -

- i. mkurugenzi wa Uchaguzi anawatumia Tangazo la kuwaalika wenye sifa kuomba nafasi hizo;
- ii. mkurugenzi wa halmashauri atabandika matangazo hayo kwenye mbao za matangazo za ofisi za watendaji wa kata, mitaa na vijiji kwenye halmashauri zenu;
- iii. tangazo hilo libandikwe kuanzia tarehe 18 Aprili, 2024;
- iv. tangazo hilo litadumu kwa muda wa siku kumi kuanzia tarehe 18 Aprili, 2024 hadi tarehe 27 Aprili, 2024;
- v. waombaji watawasilisha maombi yao wakibainisha kazi wanayoomba kama ni Mwandishi Msaidizi au Mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki (BVR Kit Operator);
- vi. mwombaji atapaswa kuthibitisha ukaazi wake kwenye kata husika kwa kupata uthibitisho huo kutoka kwa afisa mtendaji wa kijiji / mtaa;
- vii. mtendaji wa kata atapokea maombi ya barua bila kufungua barua za maombi na kuziwasilisha kwa mkurugenzi wa halmashauri tarehe 28 Aprili, 2024;
- viii. mkurugenzi wa halmashauri atazifungua na kuingiza taarifa za kila mwombaji kwa kuzingatia fomati iliyoambatishwa na barua hii;
- ix. atatengea orodha ya wanaoomba nafasi ya mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki na wale walioomba nafasi ya mwandishi msaidizi;
- x. mkurugenzi wa halmashauri atatuma orodha ya waombaji wote Tume kwa kutumia barua pepe ya daniel.kalinga@inec.go.tz na cecilia.sapanjo@inec.go.tz muda wowote kuanzia tarehe 30 Aprili, 2024 hadi tarehe 02 Mei, 2024 na;
- xi. mkurugenzi wa halmashauri atatuma orodha ya waombaji iliyoandikwa kwenye fomati iliyoambatishwa bila kuambatisha barua za waombaji.

4. Pamoja na barua hii nimeambatisha Tangazo husika. Kwa mawasiliano zaidi mnaweza kuwasiliana na wafuatao;

i) Ndugu George Kashura kwa simu namba **0785825715** au barua pepe:

george.kashura@inec.go.tz


ii) Ndugu Daniel A. Kalinga kwa simu namba **0765 284406** au barua pepe:

daniel.kalinga@inec.go.tz

iii) Ndugu Cecilia Sapanjo kwa simu namba **0714 681210** au barua pepe:

cecilia.sapanjo@inec.go.tz

5. Nashukuru kwa ushirikiano wenu.



Kailima, R. K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI

**FOMATI YA KUWASILISHA MAJINA YA WAOMBAAJI WA NAFASI ZA WAANDISHI WASAIDIZI NA
WAENDESHAJI WA VIFAA VYA BAYOMETRIKI**

Mkoa:.....

Halmashauri:.....

Idadi ya Kata:.....

Jedwali Na. 1 Orodha ya waombaji wa nafasi ya Waandishi Wasaidizi

Na.	Kata	Jina la Mwombaji	Jinsi	Umri	Elimu	Matumzi ya Komyuta au Simu Janja	Namba ya Simu	Ikiwa mwombaji ni Mtumishi wa Umma andika cheo na ofisi anayofanyia kazi	Jina la Mtaa anaotoka
1.	Azania	Juma Rashidi Saidi	Me	27	Kidato cha nne	Ndiyo	0713 000 000	Mwalimu Shule ya Msingi Tegeta	Manzese

Jedwali Na. 2 Orodha ya waombaji wa nafasi ya Waendeshaji wa Vifaa vya Bayometriki

Na.	Kata	Jina la Mwombaji	Jinsi	Umri	Elimu	Matumzi ya Komyuta au Simu Janja	Namba ya Simu	Ikiwa mwombaji ni Mtumishi wa Umma andika cheo na ofisi anayofanyia kazi	Jina la Mtaa anaotoka
1.	Azania	Juma Rashidi Saidi	Me	27	Kidato cha nne	Ndiyo	0713 000 000	Mwalimu Shule ya Msingi Tegeta	Manzese